# Wizara ya Mifugo yapanga kuboresha sekta ya mifugo

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amesema katika mwaka wa fedha 2021/22 wamepanga kuboresha sekta ya mifungo kwa kujenga majosho 129, ili kuongeza thamani ya bidhaa zitokanazo na mazao ya mifugo.

Ndaki aliyasema hayo Bungeni Dodoma wakati wizara hiyo ilipokuwa ikiwasilisha bajeti ya sekta ya mifugo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Waziri Ndaki alisema, Wizara yake imedhamiria kufanya maboresho makubwa katika sekta ya mifugo ili kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na mifugo na kuchangia pato la taifa.

Alisema eneo ambalo watalifanyia kazi ni kujenga majosho 129, mapya pamoja na kukarabati yaliyopo ili kusaidia wafugaji kupata huduma hizo katika maeneo yao.

"Tutahakikisha tunajenga majosho kwa ajili ya kuogeshea mifugo kila eneo lenye mifugo nchini, lakini pia kukarabati majosho yote yalipo ili kuwezesha wafugaji kupata huduma za ugani katika maeneo yao," alisema.

Ndaki alitaja eneo jingine ambalo watalifanyia kazi ni kuboresha eneo la malisho kwa ajili ya mifugo, ili kuwa na malisho ya uhakika na kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

"Katika hili, hivi sasa tumepunguza bei ya kukodisha maeneo ya malisho kwa kukodisha kwa sh. 3,500 kwa heka kwa mfugaji atakayehitaji eneo la malisho," alisisitiza.

Hata hivyo alisema katika mwaka huu wa fedha, wamepanga kukusanya mapato katika sekta kiasi cha sh. bilioni 50.

Awali Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayesimamia sekta ya mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel akiwasilisha bajeti ya sekta ya mifugo mbele ya kamati hiyo, alisema itasaidia kuongeza thamani ya mifugo.

Profesa Gabriel alisema katika mipango ya bajeti ijayo, wamepanga kuhakikisha wanaweka kwenye kuboresha afya ya mifugo, pamoja na kutafuta masoko ya mazao ya mifugo.

"Katika kipindi hiki, tutahakikisha tunatafuta masoko katika bidhaa za mazao ya mifugo kama vile nyama, ngozi na maziwa lakini pia kuongeza fursa nyingine ya matumizi ya vitu kama kwato, pembe na manyoya," alisema.

Hata hivyo alisema mpaka sasa wameshapata wawekezaji kutoka nchi ya Slovakia, ambao wameahidi kuja nchini kuwekeza kiwanda cha kutengeneza mbolea kwa kutumia manyoya, pembe pamoja na kwato.

Alitoa wito kwa wafugaji nchini kutumia fursa ya mitamba ya kisasa iliyopo katika ranchi za taifa, kufanya uhimilishaji ili kupata mifugo iliyobora kwa ajili iweze kuwainua kiuchumi na kuongeza pato la taifa.



**Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (kulia) akiwa na Naibu Waziri, Pauline Gekul pamoja na watumishi wa Wizara hiyo wakati wa uwasilishaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/21 na makadirio ya bajeti ijayo ya mwaka 2021/22 ya sekta ya mifugo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji iliyokutana juzi Bungeni Dodoma.** (Na Mpigapicha Wetu)

Scanned with CamScanner

# Serikali, Kampuni ya ngozi kuelimisha wafugaji

**Na Kija Elias, Moshi**

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Kampuni ya Kilimanjaro International Leather Industries Ltd, wameanza kuchukua hatua mbalimbali za kuwaelimisha wafugaji na wachunaji ngozi wa machinjio, ili waweze kuboresha kazi zao kwa kutoa mazao bora ya ngozi zitakazoingizia fedha za kigeni.

Hayo yalisemwa jana na Meneja Masoko na Mauzo wa kiwanda hicho, Donal Nkomavantu wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari waliopata fursa ya kukitembelea kiwanda hicho kilichopo nje kidogo ya mji wa Moshi.

Nkomavantu alisema, bado elimu kwa wafugaji na wachunaji ngozi wa machinjio ni ndogo hivyo kwa kulitambua hilo wao kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, wameanza kutoa mafunzo kwa kada hiyo ili waweze kuboresha kazi zao kwa kutoa mazao bora ya ngozi zitakazoingiza fedha za kigeni kutokana na mauzo ya nje na kukuza uchumi wa taifa.

Alisema kwa mwaka 2020 walitoa mafunzo kama hayo kwa Kanda ya Ziwa kwa kutoa semina kwa wafugaji na wachinjaji jinsi ya utunzaji bora wa ngozi, namna ya kuchinja na kukata ngozi hiyo ili ibaki na ubora wake unaotakiwa pindi itakapofika kuchakatwa ipatikane bidhaa bora.

Meneja huyo alisema Aprili mwaka huu, wanatarajia kuanza kutoa semina nyingine kwenye mikoa mitano iliyopo Kanda ya Kati, lengo likiwa ni kuwaelimisha wafugaji na wachinjaji juu ya uchinjaji bora wa ngozi na uhifadhi bora wa ngozi ili isipoteza ubora.

"Tanzania imekuwa ikipata kiasi kidogo cha fedha za kigeni kutokana na uharibifu wa ngozi licha ya kuwa ni nchi ya pili kwa wingi wa mifugo Barani Afrika baada Ethiopia," alisema.

Nkomavantu alisema kwa sasa, asilimia 50 ya uharibifu wa ngozi inafanyika katika machinjio hasa wakati wa uchunaji.

"Uongozi wa kiwanda tayari umejiandaa kwenye kutoa elimu hii kwa wafugaji na wachinjaji wa mifugo namna bora ya kuchinja na kutunza ngozi, ili kupata ngozi bora isiyokuwa na matundu na mafunzo haya tunatarajia kuyatoa kwa wachinjaji wote hapa nchini, ambapo tutakuwa tukienda kwa awamu katika mikoa yote nchini," alisema.

Aliongeza kuwa kiwanda hicho, pia kinakusudia kutanua soko la bidhaa zake ikiwemo viatu vya kijeshi na vile vya kiraia na bidhaa zitokanazo na ngozi kwa ubora wa kimataifa.